# Kuboreka kama Mwalimu aliye kama Kristo— Tathmini binafsi

Kama walimu, tunapaswa kila mara kutathmini uimara na udhaifu wetu ili kwamba tuweze kuwasaidia wanafunzi kujenga imani yao katika Yesu Kristo na kuzidi kuwa kama Yeye. Shughuli ifuatayo inaweza kukusaidia kutumia kanuni za kufundisha kama Kristo. Fikiria jinsi kauli zifuatazo zinavyokueleza wewe vyema kama mwalimu. Chagua jibu linalofaa sana kwa kila kauli: (1) nadra, (2) wakati mwingine, (3) mara kwa mara, (4) karibu kila mara.

Kisha, ukiongozwa na Roho, kwa maombi chagua baadhi ya vitu vichache ungetaka kuboresha. Jiwekee malengo kadhaa na utumie nyenzo hii kukusaidia kuwa bora.

## Fokasi kwa Yesu Kristo

__ Ninafundisha kuhusu Yesu Kristo haijalishi kile ninachofundisha.

__ Ninasisitizia mfano wa Yesu Kristo.

__ Ninawasaidia wanafunzi kutambua upendo, nguvu na rehema za Bwana katika maisha yao.

__ Ninawasaidia wanafunzi kuimarisha uhusiano wao na Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo.

__ Ninawasaidia wanafunzi kwa makusudi kujitahidi kuwa zaidi kama Yesu Kristo.

## Wapende Wale Unaowafundisha

__ Ninajitahidi kuwaona wanafunzi katika njia ambayo Mungu anawaona.

__ Ninatafuta kuwajua wale ninaowafundisha—ili kuelewa hali zao, mahitaji yao na uimara wao.

__ Ninasali kwa ajili ya wanafunzi kwa jina.

__ Ninabuni mazingira salama ambapo wote wanaheshimiwa na kujua michango yao inathaminiwa.

__ Ninatafuta njia sahihi za kuonyesha upendo.

## Fundisha kupitia Roho

__ Ninajiandaa binafsi kiroho ili kufundisha.

__ Ninajibu minong'ono ya kiroho kuhusu mahitaji ya wanafunzi.

__ Ninabuni mazingira na fursa kwa ajili ya wanafunzi kufundishwa na Roho Mtakatifu.

__ Ninawasaidia wanafunzi kutafuta, kutambua na kutenda juu ya ufunuo binafsi.

__ Ninatoa ushuhuda kila mara, na kuwahimiza wanafunzi kushiriki hisia zao, uzoefu wao na shuhuda zao.

## Fundisha Mafundisho

__ Ninajifunza mafundisho ya Yesu Kristo kwa ajili yangu mwenyewe.

__ Ninafundisha kutoka kwenye maandiko na maneno ya manabii wa siku za mwisho.

__ Ninawasaidia wanafunzi kutafuta, kutambua na kuelewa kweli katika maandiko.

__ Ninafokasi kwenye kweli ambazo zinaongoza kwenye uongofu na kujenga imani katika Yesu Kristo.

__ Ninawasaidia wanafunzi kupata uhusiano binafsi katika mafundisho ya Yesu Kristo.

## Alika Kujifunza kwa Bidii

__ Ninawasaidia wanafunzi kuchukua jukumu la kujifunza wenyewe.

__ Ninawahimiza wanafunzi kuja kumjua Mwokozi kwa kujifunza injili kila siku.

__ Ninawaalika wanafunzi kujiandaa kujifunza.

__ Ninawahimiza wanafunzi kushiriki kweli wanazojifunza.

__ Ninawaalika wanafunzi kuishi kile wanachojifunza.